# Dhima ya Methali za Kiswahili kwa Jamii za Kenya ni Nini?

*Joseph Nyehita Maitaria*
*Chuo Kikuu cha Karatina*

**Ikisiri**

**Methali hutokana na utamaduni wa watu na hutumika katika kuibulia na kuelekezea busara ya wenyeji. Aidha, methali za Kiswahili zimeshirikisha methali za jamii mbalimbali za Afrika Mashariki. Kwa sababu hii, zina mtazamo unaovuka mipaka ya jamii moja. Kwa sababu hii, ni mwavuli unaohifadhi na unaoibulia utamaduni asilia wa wenyeji. Methali hizo hutekeleza dhima ya uashiriaji, uelezaji na uelekezaji kuhusu maisha kwa kuzingatia 'undani' na 'upana' wa Wakenya kama jamii moja. Data ya makala hii ilitokana na methali zilizohifadhiwa katika vitabu vya methali za Kiswahili zilizokusanywa kutoka kwa wanajami wa Kenya. Methali hizo zilipata maelezo ya wanajamii wa Wakenya. Kadhalika, wataalamu wa lugha na wahakiki wa fasihi walihojiwa ili kupata fasiri za kijumla kuhusu methali. Katika uchanganuzi wa data, nadharia ya Semiotiki imetumika kubainishia viashiria na viashiriwa vya kitamaduni katika jamii za Wakenya. Kwa hivyo, makala hii inaeleza namna methali hizo zinavyoweza kutumiwa kwa ufaafu zaidi kwa jamii za Kenya.**

**Maneno Muhimu**: Dhima, Methali, Kiswahili, Jamii, Kenya

## Utangulizi

Kutokana na maendeleo ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya, dhima za lugha za kwanza zimekuwa zikitekelezwa kwa lugha hii. Tukio hili hilola hiari na limechangia pakubwa katika matumizi na uenezwaji wa methali za Kiswahili[1]. Kwa hivyo, methali za Kiswahili ni kiwakilishi na daraja muhimu ambalo linalowaunganisha wanajamii wenye asili tofauti tofauti nchini Kenya. Kauli zinazothaminiwa zaidi ndizo zitumiwazo katika uhifadhi na ubainishaji wa falsafa za wenyeji. Kauli hizo hutumiwa kama chombo cha kushirikisha na kufafanulia mitazamo ya kitaifa, kikanda na kimaeneo (Maitaria, 2019). Kadhalika, jamii huundwa kwa tamathali za usemi kwa azma ya kuwasilisha jumbe muhimu na kwa njia fiche. Kwa mantiki hii, methali za Kiswahili ni viashiria vinavyojenga taswira kuhusu maisha ya watu. Kwa makusudi, watu hutumia methali kuwasilisha fikra, imani, na mielekeo yao inayoakisi utamaduni wao (Wanjohi, 2008; Madumulla, 1995). Kwa maana hii, methali zinaweza kuwa mojawapo ya vigezo katika

[1] Methali za Kiswahili ni mkusanyiko wa methali zinazotokana na jamii mbalimbali kupitia kwa tafsiri.

kutambulisha na kushirikisha vikundi vya watu wenye asili moja. Sababu ni kwamba, methali haziibuki katika ombwe tupu bali hutokana na mazingira halisi ya jamii.[2] Hivyo, methali za Kiswahili ni chombo kinachotumiwa mno katika jamii mbalimbali nchini Kenya.

Nchini Kenya, baadhi ya kauli muhimu zinazotokana na jamii mbalimbali zimeshirikishwa kwa kuzingatia methali za Kiswahili. Kenya ni taifa linalojumuisha zaidi ya makabila 42 (Mbaabu, 1996). Kwa kushirikishwa kwa tamaduni asilia za jamii hizo; methali kutoka kwa jamii hizo zimeweza kutafsiriwa na kuingizwa kwenye matumizi ya jumla ya lugha ya Kiswahili.[3] Katika muktadha huu, hakuna jamii-lugha inayojihisi kutengwa, kusahaulika, kupuuzwa wala kuvunjiwa hadhi. Methali za Kiswahili zitaeleweka kuwa ni kauli teule zinazotumiwa kama nembo inayotambulisha utamaduni wa wanajamii. Miongoni mwa masuala yanayofafanuliwa katika makala hii ni jinsi methali hizo zinavyoashiria maono, utu, ukarimu, utangamano, malezi ya watoto, unyumba na maelekezo muhimu yanayotokana na utamaduni wa Wakenya.

Data ya makala haya ilitokana na usomaji wa methali zilizohifadhiwa katika vitabu teule vya methali za Kiswahili zilizokusanywa kutoka Afrika Mashariki. Baadhi ya methali zilizotafsirwa zilitokana na jamii za Wakenya na kupata maelezo ya wasailiwa teule. Kadhalika, wataalamu watano wa lugha na fasihi kutoka vyuo vikuu walihojiwa ili kupata fasiri za kijumla kuhusu methali za Kiswahili na mawasiliano ya wanajamii wenye asili tofauti tofauti. Data zilizopatikana zilichanganuliwa kwa kutumia nadharia ya Semiotiki. Sababu ni kwamba, methali ni kauli zenye miundo maalum na maana zake hutokana na kile kinachoashiriwa katika utamaduni wa wenyeji.

Nadharia ya Semiotiki ilipata umaarufu baada ya udhaifu wa wanamiundo kudhihirishwa kuanzia mwaka wa 1970. Kwa mfano, baadhi ya wanamiundo walijikita zaidi katika kuhakiki na kufafanua miundo ya lugha iliyotumika katika mawasiliano ya kijamii badala ya kubainisha wazi uwiano uliopo baina ya matumizi ya miundo hiyo kama ishara na kile ambacho huwakilishwa katika utamaduni wa jamii (Peck na Coyle, 1984; Hawkes, 1977 na Pierce, 1977). Kwa mujibu wa Scholes (1982), nadharia ya Semiotiki si ngeni bali ilidokezewa mwanzoni na mwanaisimu De Saussure (1916). Kadhalika, misingi na mihimili yake iliweza kufafanuliwa kwa uwazi zaidi na Pierce (1977). Kwa mujibu wa De Saussure, lugha ni mfumo wa ishara. Katika mawasiliano ya watu, kauli teule hutokana na utamaduni wa jamii. Nadharia ya Semiotiki iliweza kutumiwa mwanzoni mwa miaka ya 1960, ambapo Jakobson (1960) alibainisha vipengele sita vinavyohusu

[2] Jumuiya inayorejewa kwa enzi ya sasa ni ile ya Wakenya wanaowakilishwa kupitia kwa lugha ya Kiswahili.

[3] Kwa mifano zaidi, tazama ya methali katika Maitaria (2018), Salla (2014), Madumulla (1995), Ndalu na King'ei (1989), Ngole na Honero (1982) na Farsi (1958).

utamaduni katika mazungumzo ya watu. Vipengele hivyo ni: msemaji, mpokezi, muktadha, matini, utanzu na lugha inayoibainisha zaidi dhana ya kiashiria kama yenye yambwa na kifasiri. Katika mwaka wa 1977, Pierce aliendeleza mawazo ya Jakobson (keshatajwa) kwamba kila ishara, yaani matumizi ya matini au kitendo cha kijamii huweza kuchochea tafakuri ya kurejelea au kupatanisha na muktadha wa utamaduni na uhalisi wa jamii. Kilichosisitizwa ni kwamba, viashiria vinavyotumiwa katika jamii huwa vimejengwa katika misingi ya kufafanuliwa na kufasiriwa. Kwa hivyo, matumizi hayo hayawezi kutenganishwa na miktadha ya utamaduni na uhalisi wa jamii. Kwa kurejelea ufafanuzi wa Pierce imebainika kwamba, viashiria mahususi vya lugha kama vile methali vilivyojengwa katika tamathali za usemi hutumika mno katika mawasiliano ya jamii. Kwa hivyo, kauli hizo teule huakisi maana dhahiri na batini. Kwa maana hii, methali ni kauli teule zinazoweza kufasirika kwa namna mbalimbali kutegemea maana inayohusishwa na utamaduni wa watu.

**Dhima ya Matumzi ya Methali katika Jamii**

Methali za Kiswahili ni miongoni mwa semi zinahusishwa na utamaduni wa wenyeji wa Afrika mashariki. Hivyo, ni viishara - elekezi vya viashiria - elekezwa vya uhalisi wa jamii (Pierce, 1977; Amory, 1985). Ingawa methali ni kauli za kimapokeo, hutumika zaidi kuhifadhi na kuwasilisha falsafa ya jamii. Aidha, falsafa ya wenyeji inayowasilishwa kupitia methali huathiriwa kutokana na mabadiliko ya maisha na utamaduni katika jamii. Mabadiliko yanapojiri, methali zinaweza kufanyiwa marekebisho ili kuendana na mabadiliko hayo (taz. Omari, 2016). Marekebisho hayo hayavizi maana ya msingi katika kauli asilia. Katika mantiki hii, methali ni kauli hai zinazotumiwa kwa namna mbalimbali ili kubainisha uhalisi wa maisha na uonoulimwengu wa watu.

Ili kuakisi ujumbe unaokusudiwa, kuna haja ya kuwa makini katika uteuzi na matumizi ya methali zinazohusishwa. Hoja muhimu ni kwamba, baadhi ya methali huzungumzia wazo moja lakini kwa utofauti, usawe, unyume au kwa ukinzano kama vile: 'Pole pole ndio mwendo' na, 'Haraka haraka haina baraka'; 'Mumewe mama ni baba' na 'Mkewe baba ni mama'; 'Mama wa kambo si mama' na 'Baba wa kambo si baba' au 'Mvumilivu hula mbivu' na 'Subira huvuta heri'. Tofauti hapa ni za kimtindo unaozipa nguvu jumbe zinazopitishwa katika jamii. Usipochunguza kwa kina mweleko huu unaweza kujenga dhana kuwa, methali za Kiswahili hazina uwezo wa kujisimamia katika uwasilishaji wa ujumbe kimantiki. Kwa wageni wasioufahamu utamaduni wa jamii huweza kuchukulia kuwa, methali za Kiswahili ni kauli zinazojifunga silisili katika sheria zinazokwaza mawasiliano. Kadhalika, baadhi ya watu ambao ni 'wachanga' wa lugha ya Kiswahili huchukulia kuwa methali hazina umuhimu ila kwa akina 'yakhe'[4]. Mwelekeo huu haufifishi dhima ya kauli hizo katika kuendeleza utamaduni na falsafa ya Wakenya kama

[44] Hawa watu ambao wanadharauliwa bila sababu yoyote ya kimsingi katika jamii.

jamii. Hii inatokana na sitiari zinazoundiwa katika methali hizo (Madumulla, 1995; Finnegan, 1970). Aidha, ni rahisi kwa mtu kufahamu maana ya methali za Kiswahili kwa kuzingatia mahusiano ya maneno yaliyotumiwa (Maitaria, 2018a). Tofauti na kauli nyinginezo kama vile nahau na misemo inayotumiwa katika mawasiliano; kuna umuhimu wa kuzingatia zaidi iktisadi ya maneno yaliyopo. Kwa mtazamo huu, kuna haja ya kuzingatia umakini wakati wa kuteua na kutumia methali ili kuwasilisha maana iliyokusudiwa.

**Dhima za Methali za Kiswahili katika Jamii**

Kutokana busara zinazofumbwa kwenye methali za Kiswahili, kuna uwasilishwaji wa maarifa kuhusu namna ya kufikia ndoto 'kubwa' ya wenyeji Wakenya. Hali hii imetokana na methali za Kiswahili kuwa kurunzi ya maarifa mbalimbali katika jamii (Maitaria, 2019). Kwa mantiki hii, methali huufumba kwa ubunifu ukweli kuhusu maisha ya watu katika jamii. Hivyo, watu wanapowasilisha jambo muhimu, hawasiti kutanguliza, 'Wahenga hawakukosea waliposema…' (Nyariki, 2014: 21). Wahenga ni wazee waliostahiwa katika jamii ya Waafrika. Methali zinapotumiwa katika mawasiliano ya watu zinahusisha maana mbili: ya kijuujuu (ya kijumla inayoelea) na ya ndani (finyu au ile husishi katika miktadha ya mawasiliano). Maana iliyo wazi huzingatia miundo ya maneno yaliyopo ingawa ile batini (maana ya ndani) huwa ni ile inayonasibishwa. Katika mawasiliano ya watu, methali za Kiswahili hutekeleza dhima ya kuusawiri na kuubainisha zaidi ujumbe kwa kuwasilishwa kwa njia ya tafakari kutokana na maneno teule yaliyotumika. Kwa maana hii, methali ni kauli muhimu zinazotokana na tajriba pana na matukio maalumu katika jamii. Katika muktadha huu, 'hufichaficha' ujumbe unaodai maelezo ya kina. Isitoshe, methali nyingi zinazotokana na jamii za Kiafrika huwa zinawasilishwa kwa mafumbo au kwa kuzingatia ujazanda uliomo. Kwa mantiki hii, methali za Kiswahili hujitoa katika ufinyu wa kimaana unaohitaji utafakari na uhusishaji wa maana msingi na ile nashibishwa. Methali zinazotumiwa katika mazungumzo ya ana kwa ana ni fupi fupi. Hizo ni zile zinazofahamika kwa urahisi katika jamii. Methali ndefu huwa hazitumiki kwa ukamilifu bali sehemu ya awali tu. Mifano ya methali hizo ni: 'Akiba si mbi, <u>ingawa ya kumbi, siku ya kivumbi huti motoni'</u>; 'Mwana mtukana nyina kuzimu enda kiona, enda pigwa mkatale na pingu za mikono nyuma na silisili za moto wa jehanamu'; 'Ukimlea mwana mwema na mui mlee' na <u>'Mwana mwema ukimpa chenga na mui mpe chelele'</u>; 'Mkata hendi mkele <u>na akenda mkele akapakia mchele jahazi tele, hurudi na upele'</u>; 'Kuku wa mkata hatagi na akitaga haangui na akiangua vifaranga huliwa na mwewe'; 'Mwenye kushiriki moyo, usorudi mtima, hufa maji pondoima na kuondoka na kilema'.

Zaidi ya mifano hiyo iliyorejelewa hapo juu, kimsingi busara ya methali haijafungika katika maudhui finyu ya kijamii, bali ni kanzi yenye mirando inayohitaji kupatanishwa na vipengele muhimu katika maisha ya watu (Wafula, 1994). Baadhi ya wahakiki wanachukulia kuwa, methali huwa na maumbo na

miundo isiyobadilika katika mawasiliano ya watu (Finnegan, 1970). Kutokana na uelekeo huo wa kijumla, baadhi ya watu huzichukulia kuwa ni kauli za 'kushindilia utamaduni wa wakati uliopita' na 'hazifai kwa wakati wa sasa'. Kimsingi, methali za Kiswahili hutumiwa jinsi zilivyo au kufanyiwa marekebisho ya kadri ili kuzijengea usasa katika kukabiliana na mabadiliko ya kitamaduni yanayojiri katika uchao (Omari, 2016; Hamidu, 2020). Kwa maana hii, methali za Kiswahili ni kihifadhi cha tamaduni za wenyeji. Umaarufu wa methali za Kiswahili katika mwingiliano wa kijamii unatokana na matumizi mapana ya lugha ya Kiswahili katika kanda ya Afrika ya Mashariki na barani Afrika kwa ujumla. Wakenya wanaotumia lugha hii huzienzi methali za Kiswahili kuwa nembo ya kujivunia utambulisho na kuwa chombo cha kufafanulia utamaduni wao. Baadhi ya methali zinazotumiwa kwa sasa huweza kuwa ni zile zilizokuwapo katika mapokeo ya jamii (Ndalu na King'ei, 1989). Hata hivyo, mawazo hayo ni ya kijumla kwa sababu methali ni kipengele hai cha lugha na huweza kutumiwa kwa namna mbili: jinsi zilivyo au kufanyiwa marekebisho ya kadiri ili kuakisi usasa katika mawasiliano ya jamii (Ndungo, 2006; Madumulla, 1995; Amory, 1985). Kilicho cha muhimu katika matumizi ya methali za Kiswahili ni mawazo yanayoibuliwa na kuwasilishwa kimuktadha. Kwa wageni wanaotaka kuufahamu ustaarabu na utamaduni wa Wakenya; kianzio ni kuzifasiri methali za Kiswahili. Zaidi ya kutumiwa kama kauli za ukolezaji wa mazungumzo, zimekuwa ni chombo kinachobeba na kinachosawiri matukio halisi ya kihistoria na yale ambayo yanaendelea kushuhudiwa katika jamii ya sasa. Hivyo, maana asili ya methali ni kurunzi ya kuwatambua wenyeji na pia kufafanulia tajriba zao. Mfano ni Muyaka wa Haji ambaye alikuwa mshairi maarufu katika jamii ya Waswahili aliibua kauli na kuzitumia na baadaye zikakubalika katika jamii. Miongoni mwa methali hizo ni 'Bara Hindi ndiko kwenye nguo na wenda uchi wako.' Methali hii inaashiria habari walizozipata wenyeji waliofika Hindi na kuajabia maisha ya jamii za Wahindi (King'ei, 2000). Ingawa methali hii inaashiria yale yaliyoyoshuhudiwa Bara Hindi, methali hiyo imefasiriwa kwa kuhusisha na maono ya jamii ya Muyaka wa Haji.

**Huwakilisha Mtazamo Mpana wa Jamii**

Katika ufasiri wa methali za Kiswahili zenye mtazamo mpana[5] katika mawasiliano ya kijamii, ni muhimu kufahamu sifa zake. Kulingana na Miruka (1999) na Lo Liyong (1972), methali katika muktadha wa wenyeji wa Afrika, huweza kugusia takribani kila kipengele cha maisha na utamaduni wao. Aidha, mawasiliano ya watu yanaweza kushirikisha matumizi ya aina mbili ya methali za Kiswahili: yale yaliyo wazi au dhima ya methali huweza kudhihirika kupitia kwa ujumbe wenye mwangwi wa methali (Maitaria, 2018b). Sababu zinazowafanya Wakenya kutumia methali za Kiswahili katika mawasiliano yao ni:

[5] Ni methali ambazo zimevuka mipaka ya kijamii, zimekubaliwa na kutumiwa kama kitambulisho cha jamii zaidi ya moja.

a) hugubika ukweli unaoweza kufafanuliwa kwa kuzingatia hali halisi ya maisha ya watu. Aidha. ni kauli zinazojenga usaili na tafakari. Mfano hapa ni methali: 'Heri jirani kuliko ndugu wa mbali'. Hi ni methali ya kawaida ambayo inahitaji kufasiriwa kwa kufahamu umuhimuwa watu hawa wawili 'jirani' na 'ndugu';
b) kauli hai zinazotumika kimuktadha katika mawasiliano ya kijamii. Aidha, zinaweza kufanyiwa marekebisho ili kuwiana na mabadiliko yanayojiri katika jamii. Mfano ni: 'Ukiona kwako kunaungua kwa mwenzako kunataketea' (ambapo inaweza kuwasilishwa: ifuatavyo: 'Ukiona kwako kumepauka kwa mwenzio kumevunjika' au Ukiona kwako kunafuka kwa mwenzo kwawaka').
c) huifaidi jamii kwa kuelekeza masuala ya kimaadili na kwa maarifa yanayohitajika kutatulia migororo sugu iliyopo katika jamii. Kwa hivyo, zinatokana na ukweli au uhalisi wa maisha ya watu. Mifano ni: 'Nazi mbovu harabu ya nzima' na 'Samaki mmoja akioza ni mtungo mzima'. Methali hizi zinalenga watu wasiozingatia mwafaka wa taratibu zilizopo katika jamii. Kwamba, mwanajamii akitenda kinyume cha matarajio ya jamii, ni jamii nzima itakayoelekezwa kidole cha lawama; na
d) zinahitaji maelelezo sahihi kutokana na utamaduni wa watu kwa kushirikisha jamii mbalimbali zenye uwiano wa kimwelekeo. Mfano ni: 'Mgaagaa na upwa hali wali mkavu'. Katika methali hii, kuna haja ya kufahamu utamaduni wa Waswahili kama jamii na dini ya Kiisilamu.

Kutokana na maelezo hayo, methali zinazotumiwa na wenyeji wa Kenya ni zile zinazohusisha na kuwakilisha mtazamo mpana wa Wakenya. Methali hizo tayari zimejitoa katika ufinyu wa ukabila. Kwa sadfa, methali ni chombo muhimu cha kujengea usemezano wa nafsi, mtu na mtu au mtu na watu na watu na watu (Wa Mutiso, 2017). Kwa hivyo, huhifadhi hekima na busara ya Wakenya na vilevile kuwa chombo cha kuwaelekeza watu katika kukabiliana na sura mbalimbali za matatizo yaliyopo katika maisha ya sasa.

**Hujenga Utamaduni wa Utu na Ukarimu katika Jamii**

Tangu mifumo ya kibepari na ubwanyenye ilipoletwa na kukita mizizi nchini Kenya kupitia kwa utawala wa kigeni au wa kikoloni; baadhi ya wenyeji wamekuwa wakipigania ubinafsi ambapo ushirika ulipewa nafasi ya pili. Methali zipo katika jamii mbalimbali nchini Kenya na wenyeji wamekuwa wakizitumia katika mawasiliano yao muhimu. Kimsingi, dhima ya methali za Kiswahili ni kuimarisha mahusiano ya 'ndani kwa ndani' katika jamii na maingiliano ya jamii moja na nyingine. Katika misingi ya utambulisho wa utamaduni mpana wa Wakenya, methali za Kiswahili (ambazo ni mwangwi wa methali zinazopatikana katika jamii nyingine nchini Kenya) zinasisitiza zaidi masuala ya wema na uhisani. Mifano ni: 'Mgeni njoo, mwenyeji apone' kwamba, wenyeji huwa wenye ukarimu wageni

wanapowazuru ambapo mifugo kama vile mbuzi, ng'ombe au hata jogoo huchinjwa kuwa kitoweo. Ukarimu na shukrani ni kitovu cha utamaduni wa Wakenya. Aliyekiuka misingi hiyo, alihisiwa kuwa adui. Suala hili pia linadhihirika kupitia methali za Kiswahili zifuatazo: 'Akomelepo mwenyeji na mgeni akomelepo hapo' na 'Asiyekosa ni malaika'; 'Baa haimpati mmoja'. Methali katika jamii ya Abaluhya ni, *'Avageni ni marara* (Wageni ni kama matawi ya mgomba) kwamba, wageni hata wakiwa wengi hukaribishwa. Makaribisho hayo ni ya kujitolea kwa muda mfupi na baadaye wageni hao huondoka. Mifano mingine ni 'Alaye peke yake hufa peke yake'; 'Jumbe asiye uji haamkiwi'; 'Mali ya bahili huliwa na wadudu' na 'Nyama choma haiwezi kuwa tamu ukimsahau aliyeichoma'. Kwa hivyo, uzingatiaji wa maswala ya shukrani na ukarimu ni mtaji wa kuwekeza katika jamii ya Waafrika. Utu na ukarimu ni miongoni mwa nguzo muhimu katika ubainishaji wa utamaduni wa Wakenya.

**Huimarisha Utangamano katika Jamii**

Matarajio ya wengi katika jamii ya sasa ni kuimarisha mahusiano mema miongoni mwa watu wanaotumia lugha mbalimbali za kijamii au za kikabila. Kuna haja ya kuvumiliana na kudumisha amani, upendo na umoja. Kauli zinazoutukuza ukabila nchini Kenya ni hatari na zinaweza kuwa kikwazo cha uthabiti, ushirikiano na maendeleo ya taifa (Wa Mutiso, 2017). Baadhi ya methali hizo ni 'Fimbo ya mbali, haiuwi nyoka', 'Heri kujenga daraja kuliko kujenga ukuta' na 'Udugu ni kufaana si kufanana'. Methali hizi zina mwelekeo bayana na chanya zikilinganishwa na 'Damu ni nzito kuliko maji' na 'Mtu hachagui ndugu'. Methali hizo ni kurunzi ya kuwaelekeza watu kujenga mwelekeo wa ujirani mwema wenye amani na umoja; ndani ya jamii moja na miongoni mwa wanajamii mbalimbali.

Nchini Kenya, kuna baadhi ya watu ambao 'hawakubahatika' katika maisha yao ykiuchumi hasa wanapolinganishwa na wengine. Hata hivyo, himizo la Wakenya ni kuishi vizuri kwa kuheshimiana bila ya kujali tofauti zao za kiuchumi na kijamii. Methali za Kiswahili zinatoa uelekezi kwa wanaojiweza kuwasaidia wale ambao hawakubahatika katika jamii. Baadhi ya methali hizo ni 'Mgaagaa na upwa hali wali mkavu' (kwamba, wale wasiojiweza kimaisha huwa wanakwenda ufukweni mwa bahari kwa matarajio (ya uhakika). Kulingana na utamaduni wa jamii ya Waswahili wavuvi wanaporejea kutoka majini watachukua samaki wakubwa wakubwa tu na kuacha samaki wadogo. Samaki hao huachwa ufuoni mwa bahari kwa matarajio kuwa, wale wasiojiweza nao wapate cha kutowelea. Katika jamii za Wakuria na Wamasai matendo hayo ya kufaana yapo pia. Wakuria[6] wanaruhusu mwenye njaa au wale wasiobahatika, kungia shambani na kuvuna mahindi madogo madogo baada ya mkulima mwenye shamba kuchukua mahindi makubwa

[6] Baadhi ya mifano imetototokana na jamii nyingine zilizopo nchini Kenya. Sababu hapa ni kueleza kwa kusisitiza kuwa, tamaduni za jamii hii na jamii na nyingine zilizopo nchini Kenya zinawiana katika masuala ya kitamaduni. Hivyo zinaweza kutafsiriwa na kwa Kiswahili na kuingizwa moja kwa moja katika Methali za Kiswahili.

makubwa. Hivyo, kuna methali kama *Mugesa mahindi make ti mwibi* 'Anayevuna mahindi madogo shambani si mwizi'. Methali hii inaeleweka katika jamii ya Wakuria kwamba, mtu mwenye njaa ana hiari ya 'kuvuna' mahindi machache kwa ajili ya chakula cha kutwa lakini si mengi ya kwenda kuuza au kwa sababu nyingine yoyote. Kadhalika, jamii ya Wamasaai wana methali inayozingatia uchinjaji ng'ombe. Kwa wale waliopo wawe wameshiriki au kutoshiriki katika zoezi hilo la uchinjaji haondoki mikono mitupu. Maelezo haya kutoka jamii nyingine yana mwangwi wake katika methali za Kiswahili zilizorejelewa hapo juu.

Kwa miaka ya sasa kumekuwapo na harakati za makusudi katika kukabiliana na sura mbalimbali za ukabila. Baadhi ya methali zenye mwono finyu wa kikabila hazitumiki hadharani kutokana na kusisitiza utangamano katika jamii moja na pia katika jamii mbalimbali zinazotagusana. Mifano ya methali hizo ni: 'Damu ni nzito kuliko maji'; 'Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe'; 'Mtoto wa nyoka ni nyoka'; na 'Samaki mmoja akioza ni mtungo mzima'. Maoni ya Sibila (2019) ni kwamba, mila ni nguzo ya jamii na kitambulisho cha kujivunia utamaduni ingawa baadhi ya mila hizo zimepitwa na wakati na zinapaswa kutupiliwa mbali na jamii kuelimishwa kuhusu athari ya mila hizo. Mataifa yanayotumia lugha moja yamekuwa yakishangazwa kwa kuwapo kwa uanuai wa lugha barani Afrika. Kila mwaka, mwezi wa Februari tarehe 21 huwa ni siku inayotengwa mahsusi kutambua na kusherehekea lugha za kwanza ulimwenguni. Siku hii inaitikia wito ulioasisiwa na UNESCO mwaka wa 2000 (Muusya, 2019). Mtazamo wa Thiong'o[7] ni kuwa, '...jamii za Ulaya kama vile Wafaransa na Waingereza wanaozingatia lugha moja tu katika mawasiliano yao; hawako katika hali nzuri kiisimu wanapolinganishwa na watu ambao wana umilisi wa lugha asilia ya wenyeji na lugha nyingine moja au zaidi'. Kutokana na athari za lugha za kigeni na utamaduni wake; mtetezi huyu na gwiji wa lugha za Kiafrika alizungumzia masuala muhimu yanayowahusu wenyeji wa Afrika kwa Kiingereza, tena katika taifa lake na katika Gatuzi la Kitui ambapo wengi wa wenyeji wanazungumza lugha ya Kikamba kama lugha yao ya asili. Maelezo yake ni kwamba, '... wenyeji wa Afrika wana umilisi wa lugha zaidi ya moja: yao asilia na lugha nyingine moja au zaidi'. Katika kuukariri ujumbe wake kuhusu umuhimu wa kuzitambua na kwa matumizi ya lugha asili za wenyeji wa Afrika alisema kuwa, '... kila ngoma ina mdundo wake ... na watu wa ulaya wanahimiza lugha zao kama vile Kiingereza inayotumiwa mbinguni ... lugha za kwanza zitukuzwe kisha zihamishiwe kwenye lugha ya Kiingereza ....' Mawazo ya mkereketwa huyu wa lugha asilia za Kiafrika ni kwamba, mwanajamii ambaye hatambui lugha yake ya kwanza ni sawa na mtumwa.

[7] Mtaalamu wa masuala ya Lugha na Fasihi za Kiafrika. Alitoa hotuba tarehe 21 Februari, 2019 katika Bewa la Kitui, Chuo Kikuu cha Kenyatta wakati wa Kuadhimisha Siku ya Lugha za Lugha- Mama Ulimwenguni.

Mawazo hayo ya wa Thiong'o (2019) yanaweza kuwa na ukweli kwa kuzingatia wanajamii wenye umilisi wa lugha moja asilia na lugha nyinginezo za kimataifa. Endapo mataifa hayo yana lugha moja; lugha hiyo iwe ile isiyohusishwa na migawanyo ya 'ndani kwa ndani' kwa kuzingatia wanajamii wenye asili mbalimbali katika taifa. Kauli ya pili ya wa Thiong'o ina mashiko zaidi kwa ambavyo inaelekeza kuwapo kwa lugha na tamaduni nyingi katika umoja. Himizo hapa ni ushirikishwaji wa makabila mbalimbali kwa kutumia lugha moja. Kulingana na Schlee na Sahado (2002:7), '...methali zinashirikisha itikadi na falsafa muhimu za wenyeji na pia jamii zenye ukuruba nazo'. Nchini Kenya, mwafaka huo unaweza kuwepo kwa kuzingatia methali za Kiswahili kama kauli muhimu zenye kushirikisha maono, itikadi na falsafa jamii mbalimbali zilizopo.

Kabla na baada ya uhuru mwaka 1964 katika taifa la Kenya, watu wamekuwa wenye mahusiano ya karibu baina ya jamii na jamii; walijitambulisha na kujitofautisha zaidi kwa misingi ya ukabila, lugha na tamaduni zao asilia. Kihistoria, wenyeji wa lugha hizo walistahi tofauti zao na mahusiano ya 'jamii na jamii' hayakuwa yenye 'mipaka'. Tofauti za wenyeji zilitambuliwa kutokana na lugha zao na Kiswahili kilitumiwa kama njia ya kusaidia kuwafikia watu wenye asili mbalimbali. Kabla ya ukoloni kuenea katika maeneo mbalimbali ya Afrika Mashariki, lugha ya Kiswahili imekuwa ikitekeleza dhima ya mawasiliano mapana miongoni mwa jamii zilizopo nchini Kenya na mataifa mengine ya Afrika Mashariki na Afrika ya Kati (Madumulla, 1995; Parker, 1974). Kiungo jumuifu ni baadhi ya kauli maalum na maarufu zilizotumiwa katika jamii hizo. Kwa sadfa, methali za Kiswahili zilizopo kwa sasa zinashirikisha falsafa na mielekeo ya wenyeji wenye tamaduni tofauti. Kwa ujumla wenyeji wa Kenya wana maono sawa kutokana na tajriba zao za maisha. Methali hizi zinatokana na mazingira ya wenyeji wa Afrika Mashariki (Maitaria, 2018a; Salla, 2014). Kwa sababu hii, baadhi ya methali zinafafanuliwa na zinafasiriwa kwa upatanisho wa miktadha anuwai ya wenyeji wa taifa la Kenya kama mojawapo ya mataifa ya Afrika Mashariki. Kwa sababu hii, methali za Kiswahili zinaweza kufananishwa na 'tunda ambalo halijaoza'.

Kushirikishwa kwa methali katika mawasiliano ya watu wanaotumia Kiswahili ni jambo la hiari kutokana na historia inayohusu mahusiano ya wenyeji. Matokeo ni kukwasishwa kwa Kiswahili katika kuzungumzia masuala muhimu ya wanajamii. Kwa sasa, lugha ya Kiswahili imetomelewa methali zinazotokana na jamii mbalimbali zilizopo. Hivyo, ni vigumu kufahamu asili ya baadhi ya methali ila kupitia kwa tafiti za kina kuhusu chimbuko lake. Hapa ieleweke kuwa, si methali zote za jamii ambazo hupata mwanya wa kuchopekwa katika lugha hii bali ni zile zinazotekeleza dhima chanya. Methali hizo ni zile zinazoonya, zinazokashifu na zinazojenga maridhiano ya kustahiana katika jamii. Baadhi ya watu wamekuwa wakizichukulia methali zenye kukashifu matendo yanayokiuka utamaduni wa jamii, kuwa zina mwelekeo hasi ambapo sivyo (Maitaria, 2018b). Hata hivyo, kuwapo kwa methali kama kauli muhimu katika lugha ya Kiswahili kumesaidia kushirikisha

jamii mbalimbali kuwa moja katika taifa la Kenya. Zile zinazojibainisha katika maono finyu, ni nadra kutumika hadharani na hujitokeza kama sajili katika mawasiliano ya watu. Watu wanaotumia methali hizo, hudharauliwa kutokana na uashiriaji wa ukabila. Kwa misingi hii, methali za Kiswahili ni kioo cha kuthamini na kufahamu utamaduni wa jamii pana ya Afrika (Gesero, 2009). Kwa hivyo, methali hizo hueleweka katika mazingira ya Afrika Mashariki. Methali hizo zinapohakikiwa nje ya muktadha wa wenyeji, ni kupata vivuli au maana ya kijumla isiyojikita katika utamaduni ulioziibua. Methali ni mojawapo ya vipengele muhimu vya lugha na katu haziwezi kutenganishwa na utamaduni uliozizaa, kuzilea na kustawisha matumizi yazo katika mawasiliano ya jamii. Endapo wanaoshiriki mawasiliano yanayohusisha methali hawatazingatia muktadha ulioziibua; fasiri zitatindikiwa katika kuwasilisha taswira halisi kuhusu maisha ya wenyeji. Kwa sasa, methali za Kiswahili kama kauli muhimu haziegemezwi kwenye ufinyu wa kijamii bali huwa ni vielelezo kuhusu jamii pana ya watu. Hizi ni kauli za 'sikutambui kama huniheshimu'.

Kwa kiwango fulani, falsafa katika jamii za Afrika hutokana na uwiano wa tajriba. Watu hutumia methali siyo tu kama vito vya kurembesha mazungumzo bali huwa ni vichujio vya kubainishia utamaduni wa watu. Kwa kuzingatia usanaa uliofumbwa, methali zinakuwa ni kongamano la tamathali za usemi kutokana na tajriba au umapokeo wa utamaduni wao. Hivyo, methali hutumiwa kujenga mazingira halisi yanayofahamika kwa umithilishaji unaojikita kwenye taswira, tashibihi na isitiari (Wango, 2009; Ligami na Barasa, 2006). Kwa maana hii, methali za Kiswahili huwa na maana-msingi yenye maana-vivuli. Katika muktadha huu, kila jambo lililowahi kutokea au lile lililopo hupata mshabaha wake katika methali zinazotumiwa kwa sasa. Jambo la muhimu hapa ni kwamba, methali za Kiswahili japo huchukuliwa kwa ujumla kuwa ni kauli za jadi bado zinaendelea kuwa muhimu katika kizazi cha sasa nchini Kenya.

**Hudhibiti Tamaa kwa Wanajamii**

Katika tamaduni za wenyeji wa Kenya, suala la ukarimu limekuwa likipewa kipaumbele katika mahusiano ya watu. Katika jamii ya sasa, kuna baadhi ya watu wanaoukiuka uzingatiaji wa utamaduni huu. Mwelekeo huo hasi unapozingatiwa, aghalabu watu huweza kukosekana udugu, kujenga cheche za tuhuma na mazingira ya ubinafsi miongoni mwao. Mtu anapoelekezwa kwa tamaa, huweza kujiingiza katika mambo au matendo yanayokiuka misingi ya utu kama au ujirani mwema kama vile wizi, ujambazi, kuoneana imani au wivu. Kwa kuzingatia hayo, baadhi ya watu katika jamii ya sasa wanapokosa walichokitarajia katika maisha huishi maisha ya kinjozi, wasiwasi na aghalabu huweza kupoteza mwelekeo katika maisha. Kimsingi, mtu au watu wanapaswa kuridhika kwa kile kinachowezekena kutegemea uwezo uliopo. Shime ni kujitahidi kwa kuzingatia njia zilizo halali, la sivyo mhusika hujipata katika mkono mbaya wa sheria za nchi. Katika utamaduni wa jamii za Afrika Mashariki, hasa kabla ya majilio ya wageni na mfumo wa kikoloni

na katika karne kumi na tisa; watu waliishi kwa kusaidiana bila ya kuelekezwa kwa ubinafsi wala tamaa (Wango, 2009). Methali zilikuwapo na zilitumiwa kuwakemea na kuwaonya watu dhidi ya kutotosheka au kutoridhika. Miongoni mwa methali zilizotumika ni kama: 'Ukikosa shukuru, kupata kuna Mungu'. Methali kama hiyo ilibuniwa kutokana na imani iliyojengwa katika utamaduni wa watu. Kwamba, kuna uwezo au nguvu fulani zilizozidi zile za binadamu. Nguvu hizo ndizo zilizotegemewa zaidi katika kuelekeza maisha na mafanikio ya watu katika jamii. Kwa kuzingatia uhalisi huo wa maisha, kuna kupata na pia kuna kukosa. Hayo ni baadhi ya mambo yasiyoweza kuepukika katika uhalisia wa maisha ya watu. Matumizi ya methali hiyo iliwataka watu kuishi maisha ya amani, upendo na kuheshimiana katika jamii. Kinachobainishwa katika methali hiyo ni kwamba, mtu anapokosa kufanikisha mambo kulingana na matarajio yake, ni vema kujipa moyo wa subira katika kujaribu siku inayofuatia. Kwa hivyo si jambo jema kwa mtu anapokosa kuanza kutoa malalamishi yasiyoweza kumuauni.

Katika wakati wa sasa, baadhi ya watu wamekuwa wakielekezwa zaidi kwa tamaa au ubinafsi. Hilo huwafanya watu kukosa mwelekeo na matumaini katika maisha na matokeo ni kujiingiza katika shughuli zinazotarajiwa kuwaletea tija au faida ya haraka. Kwa kufanya hivyo, hujitesa kimawazo na kuudhalilisha mwili. Kupitia kwa busara iliyofumbwa kwenye methali hiyo, watu walipaswa kuzingatia zaidi subira katika kukabiliana na harakati za maisha. Jamii ya sasa huweza kupata uelekezi wa kujiepushia mazonge au nakama ya maisha hasa kwa kuzingatia hekima inayoibuliwa katika methali hiyo. Methali nyingine ambazo pia hutoa ujumbe kama huo ni: 'Haraka haraka haina Baraka'; 'Kupa ni kumpa anayekupa, kumpa asiyekupa ni kutupa'; 'Mpanda farasi wawili hupasuka msamba'; 'Mshika mawili, moja humponyoka'; 'Mwangaza mbili moja humponyoka' na 'Karamu mbili zilimshinda fisi kuzila' (Methali hizi zinajitokeza katika jamii mbalimbali zilizopo Kenya na zinaendelezwa kwa lugha za makabila yao). Kinachobainika katika matumizi ya methali hizo ni kwamba, zimetokana na mambo ambayo yameweza kushuhudiwa katika tajriba za uhalisi wa maisha ya watu.

**Huhimiza Utamaduni wa Kufanya Kazi katika Jamii**

Kwa Wakenya kazi ni muhimu; iwe ni ya ujasiriamali au ya kuajiriwa. Kilicho cha muhimu ni kujipatia riziki kwa njia halali. Kwa kuzingatia methali za Kiswahili, kazi ndiyo inayoubainisha utu wa mtu. Watu wamekuwa wakihimizwa kutozingatia uzembe ili kuboresha, kututumua au kuinua kiwango chao cha maisha, kwa watu ambao walizembea, walibezwa, walikemewa na kudharauliwa katika jamii. Jamii ya Wakikuyu (wanapatikana katika eneo la Mkoa wa Kati, Kenya) wana methali 'Mĩcĩĩ nĩ kũrãrwõ, tĩ gũtĩndwõ'[8] (Nyumba ni pahali pa kulala si pa kushinda kutwa).

[8] Huu ni mfano wa methali katika jamii moja kama ilivyoelezwa hapo awalli kuhusu Wakuria. Umuhimu ni kuelezea kuwa, baadhi ya methali zenye kujenga utangamano wa kijamii nchini Kenya huweza kutafsirwa na kukubaliwa katika methali za Kiswahili.

Methali hii ina maana kuwa, kutwa mtu anatarajiwa kufanya kazi na wala si kustarehe (Wango, 2009; Wanjohi, 2008). Katika utamaduni wa wenyeji wa Kenya, mtu anayejitahidi kuifanya kazi, ingawa ndogo kwa kiwango chake, hupongezwa na kuhimizwa ajitahidi zaidi kwa wakati uliopo na pia kwa wakati ujao. Suala la kujitahidi katika kazi lilikuwa si la mjadala. Katika uhalisi wa maisha, ambapo ndiyo chemichemi ya methali zilizokuwapo katika jamii, ilibainika kuwa mtu asipofanya kazi hakuweza kulimudu au kulibingirisha gurudumu la maisha. Katika muktadha huu, watu walitiana shime na kuhimizana kupitia kwa methali zilizopo katika utamaduni wao, kama vile inavyodhihirishwa kwa methali ‘Ukiona vyaelea, vimeundwa’. Mifano mingine ya methali zinazoweza kutumiwa katika kuwahimiza watu kufanya kazi kwa wakati wa sasa ni kama: ‘Akutanguliaye chanoni, hukuzidi tonge’; ‘Kula uhondo kwataka matendo’; ‘Mali ya urithi haina Baraka’; ‘Mpanda ovyo hula ovyo’ na ‘Ukilala na mambo yatalala’.

Suala la ufanyaji kazi katika jamii ni jambo ambalo linahimizwa katika tamaduni mbalimbali zilizopo nchini Kenya. Utamaduni kuhusu ufanyaji kazi katika jamii mbalimbali nchini Kenya unabainishwa zaidi katika methali za Kiswahili.

**Hutanabahisha Wanajamii**

Kupitia kwa baadhi ya methali za Kiswahili zilizopo katika jamii, mandhari ya kujisaili au kutafakari na kufikia uamuzi unaofaa umeanza kujengwa. Mtu au watu wanahitaji kufanya maamuzi mwafaka kuhusu hatua inayostahili kuchukuliwa (Mtesigwa, 1989; Lo Liyong, 1972). Katika jamii ya Waluo kuna methali isemayo ‘*Dhano ipuonjo nyaka tho*’ (Mtu hujifunza kutoka kwa wenzao hadi kifo). Katika methali za Kiswahili kuna mshabaha huo, ‘Mficha uchi hazai’; ‘Mganga hajigangi’ na ‘Kinyozi hajinyowi’. Ujumbe katika methali hizi ni kwamba, ushauri au suluhu hupatikana kwa wengine. Kwa hivyo, mtu anapojipata katika shida hana sababu ya kumlaumu yeyote. Kwa sababu, methali zipo na zimekuwa kama mwavuli kauli za kurejelea wakati tukio linapojitokeza. Hata hivyo, mtu anayejipata katika janga, huwa hana sababu ya kutoa udhuru au kumlaumu yeyote. Kutokana na kuwapo wa methali za Kiswahili, mwelekeo mwafaka tayari umebainishwa na umeanikwa hadharani kwa yeyote anayehitaji kujiepusha na matukio ambayo yanaweza kumwathiri. Kimsingi, methali zimekuwapo tangu awali katika utamaduni wa watu ili kuwaelekeza kuhusu utaratibu unaotarajiwa katika maisha. Utamaduni wa Mwafrika ulimchukulia mtu kuwa muhimu na shida zinazomkumba au zile anazozizua huweza kuuathiri mfumo mzima wa jamii. Katika muktadha huo, baadhi ya methali za Kiswahili zimekuwa katika mstari wa mbele kutoa tahadhari katika jamii (Hii ni kanzi ya methali ambazo zimetokana na jamii mbalimbali zilizopo Kenya). Ingawa tangu jadi methali hizo zilikuwapo, zinaweza pia kutumiwa katika kuielekeza jamii ya sasa. Kwa mfano, methali kama hizo ni: ‘Kuvuta maji ya kina kwataka wakurufunzi’ na ‘Mkono usioweza kuukata, ubusu’. Methali zingine ambazo zinaufumba ujumbe kama huo wa tahadhari kwa jamii ni kama vile: ‘Mafahali wawili hawakai zizi moja’;; ‘Ndovu wawili wakisongana ziumiazo ni

nyika'; 'Ukimkimbiza sana mjusi, atageuka nyoka'; 'Usicheze na simba, ukamtia mkono kinywani'; 'Usilolijua, ni kama usiku wa kiza' (Methali hizi zilitokana na jamii ya Wamasai na Wakuria). Kutojana na methali hizi ni kwamba, kuna haja ya kuchukua tahadhari. Kwa hivyo, methali za Kiswahili nchini Kenya husaidia kutahadharisha na kuelekezana katika jamii.

**Husaidia Malezi ya Watoto katika Jamii**

Masuala ya watoto na haki zao zimeweza kushughulikiwa katika tamaduni za jamii za Waafrika, hasa kupitia kwa baadhi ya kauli muhimu zinazotumika katika mawasiliano ya kijamii. Malezi ya watoto na vijana ni ya jamii nzima (Mlacha, 1985): Kwa mfano, swala la 'uanaharamu wa mtoto' limeshughulikiwa vilivyo katika utamaduni kupitia kwa methali za Kiswahili kama vile, 'Kitanda hakizai haramu'. Kwa mantiki hii jamii husema kuwa, 'Aliyemwoa mama ndiye baba'. Katika hali hii hakuna uanaharamu katika jamii za Afrika. Endapo mume wa mke atakuja juu kwa makeke kuwa hamfahamu mtoto huyo ataulizwa maswali ambayo ni muhali kupata majibu kama vile, 'Ulikuwa wapi wakati huo kitendo kilipokuwa kinaendelea?' Hivyo mama mzazi huondolewa lawama na zaidi ya hayo mume huyo ataelekezwa kwa kuambiwa, 'Kosa moja hailiachi mke' na 'Kosa si kosa ila kurudia kosa'. Katika muktadha huu, mtoto hupata malezi katika mazingira ya kifamilia.

Isitoshe, wazazi hupata maelekezo ya majukumu yao kwa wana wao. Katika utamaduni wa jamii ya Wakuria, endapo wazazi watatelekeza majukumu yao kwa mtoto; jukumu hilo huwaendea watu katika ukoo wao. Methali nyingine zinazosetiri ujumbe kama huo ni: 'Dua mbaya, haombolezwi mwana', kwamba mtoto ni mtoto na anatarajiwa kutendewa yanayopaswa kama mwanajamii mwingine. Mfano mwingine ni: 'Mume wa mama, ni baba'. Maelezo hapa ni kwamba, katika utamaduni wa wenyeji, huenda mke akawa amepata mtoto kabla ya ndoa. Mwana huyu hutahadharishwa kuwa ni sharti ampe heshima yule bwana ambaye ni mume wa mama yake; 'Kila mtoto na koja lake' kwamba, kila mtoto katika jamii ana bahati yake; 'Mwenye kumchukia mwanawe, ni hasidi wa rohoye'. Kwamba, hakuna haja ya kujenga mazingira ya kumchukia au kumbagua mtoto. Hivyo, wazazi wanapaswa kuwapenda wana wao kama vile wanavyojipenda.

**Huelekeza Masuala ya Unyumba na Majukumu yake katika Jamii**

Ndoa ni taasisi muhimu katika jamii za Kiafrika hata ingawa hukumbwa na misukosuko ya kila aina. Taasisi hii imekuwa ikiyumbishwa zaidi kutokana na athari za utamaduni wa kigeni au mabadiliko ya maisha. Kutokana na hilo, jamii ya sasa imekuwa na mitazamo tofauti tofauti kuhusu namna ya kuyashughulikia masuala hayo. Hata hivyo methali zimekuwepo katika mapokeo ya utamaduni wa jamii ambazo zimekuwa zikibainisha taswira mbalimbali kuhusu mwanamke. Baadhi ya taswira hizo zimekuwa zikichukuliwa kwa kurunzi ya maisha ya sasa bila ya kuzingatia mfumo ya kiuchumi, utamaduni wa watu na uhalisi wa maisha ya wanaohusika.

Kabla ya kuzitolea misimamo ya kimwelekeo methali hizo ni muhimu kuzingatia mahusiano ya watu yalikuwaje katika vipindi mbalimbali vya kihistoria. Ikichukuliwa kuwa mwanamke alikuwa ni kivuli cha mwanamume na kwamba alikuwa akinyanyaswa itakuwa ni mtazamo finyu. Isitoshe, methali hizo hueleweka zaidi kwa kuzingatia miktadha ya utamaduni unaorejelewa na si vinginevyo. Baadhi ya kauli zinazojenga utata katika ufasiri ni kama vile: 'Mume ni kazi; Mke ni nguo, mgomba ni kupalilia'; 'Mke kipofu huwa mwaminifu' na 'Mke ni sawa na mwana' (Mifano ya methali hizi inatokana na utamaduni wa jamii ya Waswahili wanapatikana pwani ya Kenya). Mantiki ya kauli hizo zilitokana na muktadha wa utamaduni wa wenyeji la sivyo fasiri zisizofaa huweza kushehenezwa jamii za Afrika kuwa zinainyanyasa jumuiya ya wanawake. Baadhi ya wasomi wa kike wamekuwa na msimamo mkali kuhusu kauli kama hizi ambapo wanashikilia kuwa, kauli hizo zinazomlenga mwanamke hazimpi nguvu ya kukabiliana na maisha ya kijamii, kisiasa na kiuchumi (Ndungo, 2006). Mitazamo yao ni kwamba, jumuiya ya wanawake imekuwa ikidhalilishwa kama 'viumbe vya kujiegemeza' kwa mwanamume. Mielekeo hiyo haikutilia maanani utamaduni wa Mwafrika. Isitoshe, kila mtu alifahamu nafasi yake katika jamii pasi na kuhisi kudhulumiwa.

Baadhi ya methali ambazo zinaweza kutumiwa ni kama vile: 'Mke wa kwanza ni mama'. Methali hii huchukulia kuwa mke wa kwanza aliyeolewa anapaswa kupewa hadhi ya 'mama' na kuheshimiwa na wale wanaokuja baada yake. Muktadha unaosawiriwa hapa ni ule wa utamaduni wa Waafrika unaoruhusu ukewenza. Kwa hivyo, onyo hutolewa kwa 'wake wadogo' kwamba, wanapoletwa katika boma wafahamu kuwa yule aliyetangulia kuolewa anahitaji kuwekewa heshima yake. Methali hii haikuelekezwa kwa wake hao wa baadaye bali pia kwa mume kwamba, huyu wa awali ndiye hasa wa ujana wake waliyeanza naye maisha ya kimji. Baadhi ya wanaume wanapooa wake wengine husahau majukumu yao ya ndoa na kuhamia katika 'nyumba ndogo' hadi pale wanapopata masaibu ya upweke na maisha. Methali nyingine ambazo pia zinabainisha masuala ya unyumba katika utamaduni wa Mwafrika ni kama vile: 'Kosa moja, haliachi mke'; 'Mke, ni dada mdogo' na 'Ukipenda uyoga, penda na kichuguu'. Methali hizi zinatumika mno katika tamaduni za jamii mbalimbali nchini Kenya kwa lengo la kuleta utangamano wa kijamii kuhusu masuala ya ndoa na familia.

**Hitimisho**

Wenyeji wa Kenya wamekuwa wakiishi kindugu na kustahiana kwa kutambua tofauti zao za kitamaduni. Maadamu lugha ya Kiswahili imeendelea kupanua mawanda yake na kuwavutia wasemaji wengi, methali zake pia zinapata mwanya kuwasilisha utamaduni wa wenyeji wa Afrika Mashariki. Kimatumizi, fafanuzi mwafaka wa methali za Kiswahili ni uzingatiaji wa muktadha na utamaduni ulioziibua. Katika muktadha wa taifa la Kenya, methali kutoka kwa jamii mbalimbali zimeweza kuhusishwa katika hazina ya methali za Kiswahili. Katika mazingira haya methali hizo zinaweza kuwa kitambulisho cha Wakenya. Mawazo

ya kijumla yanayopaswa kuondolewa katika bongo za watu ni kama vile, methali za Kiswahili zina malengo ya 'kuwaendea wakina yakhe' ambao hawakubahatika kupata elimu ya darasani. Nchini Kenya, methali ni miongoni mwa kauli muhimu zinazotumiwa katika kubainisha uhalisi wa maisha ya sasa. Kupitia kwa methali hizo, wenyeji wa Kenya watajifunza maarifa mbalimbali katika harakati ya kusuluhishia baadhi ya matatizo yanayodumaza maendeleo ya taifa. Kadhalika, pendekezo ni kuwa baadhi ya semi kama vile nahau, vitendawili na misimo ya Kiswahili zinavyoweza kufanyiwa utafiti zaidi ili kudhihirisha jinsi zinavyotumika kuwasilishia utamaduni Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla.

**Marejeleo**


Amory, D. (1985). "Kanga Cloth and Swahili Society, Mke ni Nguo". Tasnifu ya Uzamifu, Kikuu cha Yale. (Haijachapishwa).

Ayodi, N.K. (2017). "Tafsiri na Fasiri ya Methali za Kimaragoli: Hazina katika Fasihi ya Kiafrika". Katika *Lugha na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja*. Eldoret: MUP, kur. 327-334.

De Saussure, F. (1916). *Course de Linguistique Générale*. Paris: Payot. (Tafsiri ya Kiingereza - 1959 *Course in General Linguistics*. New York: McGraw-Hill).

De Saussure, F. de. (1916). *Course de Linguistique Générale*. Paris: Payot. (Tafsiri ya Kiingereza - 1959 - *Course in General Linguistics*. New York: McGraw-Hill).

Farsi, S. (1958). *Swahili Sayings*. Nairobi: KLB.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. London: OUP.

Gesero, W.C. (2009). *Methali za Kiswahili Afrika Mashariki na Kati*. Dar es Salaam: ABSIT.

Hamidu, F. (2020). Mtindo katika Methali za Kiswahili za Kimajaribio. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa).

Hawkes, T. (1977).*The Structuralism and Semiotics*. London: Methuen.

Jakobson, R. (1960). "Concluding Statement: Linguistics and Poetics". Katika Seboek, J. (Mhr.), *Style and Language*. Cambridge: MIT. kur. 184-214.

King'ei, K. (2000). "Aspects of Autobiography in the Classical Kiswahili Poetry". Katika makala yaliyowasilishwa katika Kongamnao la ISFNR 2000 Conference, Chuo Kikuu cha Kenyatta Julai 17-22, 2000.

Ligami, P. na Barasa, S. (2001). "Tahakiki ya Methali za Kiswahili", katika Njogu, K., Momanyi, C. na Mathooko, M. (Wah.) *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi: Taweza Communications.

Lo Liyong, T. (1972). *Popular Culture of East Africa*. Nairobi: Longman.

Madumulla, J.S. (1995). *Proverbs and Sayings: Theory and Practice*. Dar es Salaam: TUKI.

Maitaria, J.N. (2018a). "Methali za Kiswahili katika Kukabiliana na Ufisadi Nchini Kenya". Katika Kandagor, M., Ogechi, N. & Mukuthuria, M (wahr.) *Mwanga wa Lugha* Juzuu la. 2 Na.1. Jarida la Chuo Kikuu cha Moi. Eldoret: MUP. kur. 57-68.

Maitaria, J.N. (2018b). "Utafiti katika Methali za Kiswahili". Katika Kandagor, M. (wah.), *Fasihi ya Kiswahili na Maendeleo yake*. Dar es Salaam: TATAKI. (kur. 121-142).

Maitaria, J.N. (2019). "Dhima ya Methali katika Kupunguza Ukabila Nchini Kenya". Katika Kobia, J., Kandagor, M., Mwita, L.C., Maitaria J.N & Wandera, S. (wahr.), *Lugha na*

Mbaabu, I. (1996). *Language Policy in East Africa*. Nairobi: Education Research and Miruka, O. (1999). *Studying Oral Literature*. Nairobi: Acacia Publishers.

Mlacha, S.A.K. (1985). "Dhima ya Methali katika Malezi". Katika *Kiswahili,* Juzuu la 52/1 na 52/2. Dar es Salaam: TUKI. kur 175-186.

Mtesigwa, P.C.K. (1989). "Methali ni Nini?" Katika *Kiswahili* Juzuu la 56. Dar es Salaam: TUKI. kur 1-9.

Muusya, J.K. (2019). "Msimamo wa Ngugi kuhusu Lugha za Kiafrika Unaegemea Pato". Safu ya Lugha na Fasihi, *Taifa Leo,* Machi 18, 2019: uk. 21. Nairobi: Nation Media Group.

Ndalu, A. na King'ei, K.G. (1989). *Kamusi ya Methali za Kiswahili.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Ndungo, C. (2006). "Matumizi ya Tamathali za Usemi katika Lugha ya Kisiasa". Katika Njogu, K. na wenzake (wah.) *Fasihi simulizi ya Kiswahili*. Nairobi: Twaweza Communications.

Ngole, S.Y.A. na L. Honero. (Wahr.). (1982): *Fasihi Simulizi ya Mtanzania: Methali*. Dar es Salaam: TUKI.

Nyariki, E. (2014).: 'Chimbuko la baadhi ya methali na misemo'.Katika *Taifa Leo Julai, 2014: 21*. Nairobi: Nation Media Group.

Omari, S. (2016). "Swahili Modern Proverbs: The Role of Literary Writers and Social Network Users." Makala katika Jarida la Swahili Forum Vol. 23 (2016), kur. 21-46.

Parker, C. A. (1974). "Aspect of Theory of Proverb". Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Washington. (Haijachapishwa).

Peck, J. na Coyle, M. (1984). *How to Study Literature, Literary terms and Criticisms*. London: MacmillanEducational Books Ltd.

Pierce, C. (1977). *Semiotics and Significs*. Bloomington: Indiana University Press.

Salla, H.D. (2014). *Methali za Kikwetu.* Dar es Salaam: Africa Proper Education Network.

Schlee, G na Sahado, K. (2002). *Rendille Proverbs in their Social and Legal Context.* Köhn: Rüdiger Köpper Verlag.

Scholes, R. (1982). *Semiotics and Interpretation*. New Haven: Yale University Press.

Sibila, S. (2019). "Tusifuate Tamaduni Potovu". Katika safu ya 'Barua kwa Mhariri', *Taifa Leo,* Machi 25, 2019: uk. 9. Nairobi: Nation Media Group.

Wa Mutiso, K. (2017). "Looking at Each Other: The Origin of Negative Ethnicity". Katika *Mwanga wa Lugha,* Juzuu 1 Na. 2 , Jarida la Chuo Kikuu cha Moi.Eldoret: MUP. kur 57-68.

Wafula, R.M. (1994). "Uainisho wa Methali". Katika *Writers Forum, A Journal of the Writers Association of Kenya Vol. 2*. Nairobi. Writers Association of Kenya.

Wango, K. (2009). *Proverbs of the Kikuyu People, Vol. 1.* Nairobi: Flame Keepers Publishers.

Wanjohi, G.J. (2008). *The Wisdom and Philosophy of Gikuyu Proverbs.* Nairobi: Nyaturima Publications.